

Mhe. Nsekela aitaka Menejimenti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kufanya kazi ndani ya mipaka yao.

Kamishna wa Maadili Mhe. Jaji (Mst.) Harold Nsekela ameitaka Menejimenti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutekeleza majukumu yake yaliyo ndani ya mipaka yake kwa kuisimamia kikamilifu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya Mwaka 1995 na Marekebisho yake.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akizungumza kwa mara ya kwanza na Menejimenti hiyo tangu alipoapishwa kushika wadhifa huo tarehe 23 Desemba, 2016.

Jaji (Mst) alisema, "tumepewa kazi kisheria, jambo letu la kwanza la msingi ni kuisimamia sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kama ilivyo."

Akitoa uzoefu wake wakati akifanya kazi katika Idara ya Mahakama Mhe. Nsekela alisema kuwa kesi ikifika mahakamani mbele ya Jaji au Hakimu wa Mahakama ya ngazi yeyote jambo la kwanza ambalo Jaji au Hakimu anatakiwa ajiulize ni kama kesi iliyo mbele yake ana mamlaka nayo kisheria kuisikiliza na kama hana mamlaka nayo anaachana nayo. Alitoa mfano huo ili kuonesha umuhimu wa kufanya kazi kwa kuzingatia mipaka kwa mujibu wa sheria.

"Ni vema tuiangalie Sheria na kuelewa mamlaka yetu ili kuepuka misugvano isiyokuwa na lazima. Kabla ya kuwaelimisha watu wengine kuhusu Sheria ya Maadili inasema nini, tuelewe sisi wenyewe na kutekeleza kama ilivyo," alifafanua Mhe. Nsekela.

Kuhusu ufinyu wa bajeti, Mhe. Nsekela aliitaka Menejimenti kuangalia vipaumbele vya taasisi vilivyo ndani ya mamlaka ya kisheria waliyonayo na kutekeleza yale yanayowezekana na kama hayawezekeani waseme hayawezekeani kwa sababu gani.

Awali akimkaribisha Kamishna wa Maadili, Katibu wa Idara ya Viongozi wa Siasa Bw. Waziri Kipacha alisema kuwa kuteuliwa kwake kunaonyesha imani aliyonayo kwake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Magufuli na kuongeza kuwa watumishi wa Sekretarieti ya Maadili watashirikiana naye katika kusimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mhe. Harold Nsekela aliapishwa kuwa Kamishna wa Maadili katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma tarehe 23 Desemba, 2016 akichukua nafasi ya Jaji (Mst) Mhe. Salome Kaganda ambaye amestaafu.